ARUSHA MEAT COMPANY LTD

P.O.BOX 14167
ARUSHA
TANZANIA
TEL: +255272970304
Mob: +255734026767
E-mail: arushameatcompany@yahoo.com

KUMB. NA. AMCL/MTNZ/78/83 **DATE: 06/11/2026.**

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Arusha Meat Company Limited inakaribisha waombaji wenye sifa za kujaza nafasi sita (06) zilizowazi kama ifuatavyo:-

1.0 MTHIBITI UBORA (QUALITY ASSURANCE OFFICER) NAFASI MOJA (1).

1.1 MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO;-

i) Kuhakikisha ubora wa bidhaa, huduma, kufuatilia utekelezaji wa viwango na taratibu za ubora.
ii) Kubaini na kutoa taarifa kuhusu kasoro za ubora wa bidhaa na huduma.
iii) Kupendekeza hatua za kurekebisha changamoto zinazohusiana na ubora wa bidhaa na huduma.
iv) Kuhakikisha sheria, kanuni na miongozo ya ubora wa bidhaa na huduma inazingatiwa.
v) Kuandaa na kutunza kumbukumbu za ukaguzi wa ubora.
vi) Kutoa ushauri kwa Menejimenti, kufatilia utekelezaji wa mapendekezo ya kuboresha ubora wa bidhaa zinazozalishwa na huduma zinazotolewa na kampuni.
vii) Kutoa elimu kwa wafanyakazi kuhusu viwango na taratibu za ubora.
viii) Kuandaa taarifa kuhusu hali ya ubora katika kampuni.
ix) Kutekeleza majukumu mengine ya kazi kama atakavyoelekezwa na Mwajiri.

2.0 MAUZO NA MASOKO (SALES –PERSONEL) – NAFASI TATU 3.

2.1 MAJUKUMU YATAKUA KAMA IFUATAVYO.

i) Kufanya mauzo ya bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na kuchakatwa na kampuni kwa wateja kwenye vitu vya mauzo (Sales Point).

ii) Kuhakikisha anafikia malengo ya siku mwezi na hatimaye mwaka kwa mauzo kadri inavyopangwa.

iii) Kuhakikisha anatoa huduma bora kwa wateja kwa kuzingatia viwango vililvyowekwa na kampuni.

iv) Kuhakikisha anapenya kwenye soko kwa kuuza bidhaa na kuitangaza kampuni sehemu mbalimbali kadiri iwezekanavyo.

v) Kufatilia na kutoa taarifaa juu ya shughuli za mauzo kwa msimamizi wake.

vi) Kupokea malalaiko ya wateja katika eneo lake la kazi na kuwasilisha kwa msimamizi Wake kwa utekelezaji ili kuweza kudumisha mahusiano mazuri kati ya mteja na kampuni.

vii) Kufatilia na kutoa taarifa juu ya shughuli za mauzo kwa msimamizi wake.

viii) Kuhakikisha usafi na mpangilio mzuri kwenye vituo vya mauzo "Sales Point" ili kuweza kuwavutia wateja.

ix) Kuhakikisha anaweka kumbukumbu sahihi za mauzo ya kila siku kwenye vitabu na mfumo wa mahesabu wa kampuni.

x) Kufanya jukumu linguine lolote atakalopangiwa na Mwajiri.

2.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

i) Awe na Stashahada (Diploma in marketing or Business Administration).

ii) Awe na uzoefu katika eneo la mauzo kwa kuitangaza biashara usiopungua mwaka mmoja na kuendelea.

iii) Awe na uwezo wa kuongea Kiswahili na kingereza kwa ufasaha.

iv) Awe na uwezo wa kutumia "Computer".

v) Awe na umri wa kuanzia miaka 21 -35.

vi) Mwombaji mwenye shahada atakuwa na sifa ya ziada "Added Advantage"

MSHAHARA.

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Arusha Meat Company Limited yaani ngazi ya **AMC3.**

3.0 MCHUNAJI (SKINNERS) NAFASI MBILI (2).

3.1 MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:-

i) Kupokea ng'ombe, mbuzi, kondoo kutoka zizini/stoo kwa ajili ya kuchinja.

ii) Kumwandaa ng'ombe, mbuzi, kondoo katika hatua ya uchinjaji.

iii) Kumsafisha ng'ombe na kumtundika/kumninginiza tayari kwa hatua ya uchunaji baada ya kuchinjwa.

iv) Kuchuna ng'ombe, mbuzi, kondoo kwa kuzingatia uchunaji sahihi usioharibu nyama wala ngozi.

v) Kutengenisha ng'ombe, mbuzi, kondoo katikati ili kuondoa ogani za ndani na kuzipeleka kwenye chumba maalum iliyotengwa na Kampuni.

vi) Kuweka alama ya nteja husika kwenye masalia yote ya ng'ombe, mbuzi, kondoo husika kwa usahihi ili kuongeza ufanisi na kuepusha kuchanganya bidhaa za wateja wa Kampuni.

vii) Kuhakikisha eneo la kazi ni safi wakati wote wa kazi.

viii) Kushiriki kufanya usafi wa jumla kwa siku zilizowekwa na uongozi wa Kampuni.

ix) Kutekeleza majukumu mengine ya kazi kama atakavyoelekezwa na wasimamizi wa kazi.

3.0 SIFA ZA MWOMBAJI.

i) Awe na leseni ya uchunaji inayotolewa na Wizara ya Mifugo.

ii) Awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha.

iii) Awe na umri kuanzia miaka 21-45

3.1 MSHAHARA.

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Arusha Meat Company Limited yaani ngazi ya **AMCL 1.**

MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZILIZOTANGAZWA.

i) Waombaji wawe raia wa Tanzania.

ii) Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa.

iii) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.

iv) Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.

v) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".

vi) "Testimonials", "provisional results", "statement of result" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**

vii) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).

viii) Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usaili.

ix) Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAPOKELEWA.**

x) Ajira hii ni ya mkataba wa muda maalum.

xi) Barua zote zielekezwe kwa;

MENEJA MKUU,

ARUSHA MEAT CO. LTD,

S.L.P 14167,

ARUSHA-TANZANIA.

xii) Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta au kwa njia ya barua pepe (email) **recruitment@arushameat.co.tz.**

xiii) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 19/11/2026.

NB: Barua zote zitakazotumwa nje ya utaratibu huu ulioelekezwa katika tangazo hili hazitafanyiwa kazi.